

RUHILA COMPANY LIMITED

P.O.BOX 80,

SONGEA-TANZANIA

TIN: 155-281-987,  **Uvccm Building Msamala, Njombe road, Email:luhiracl@gmail.com**

TANGAZO LA AJIRA

Mwenyekiti ya Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni Ruhira Company Limited anapenda kuwatangazia wenye sifa wote za kushika nafasi mbalimbali za kazi katika Kampuni hii . **LUHIRA COMPANY LIMITED** ni Kampuni ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea ambayo imesajiliwa chini ya sheria ya makampuni ya mwaka 2002.

Cheo: **Afisa Mtendaji wa Kampuni**
Mwajiri: Bodi ya Wakurugenzi
Kuwajibika kwa: Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi chairperson
Kituo cha Kazi: Songea

Kazi na Majukumu

1. Afisa Mtendaji wa kampuni atakuwa mtendaji mkuu wa shughuli zote za kampuni na masuala ya utawala ya kila siku.
2. Atawajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi kulingana na ratiba ya vikao vya bodi, kwa mwenyekiti wa Bodi au mtu yoyote atayeteuliwa na Bodi ya wakurugenzi.
3. Kuandaa mpango wa biashara wa kampuni, Mpango Mkakati na bajeti ya Kampuni.
4. Mwakilishi wa kampuni na wakurugenzi katika uendeshaji wa kampuni kila siku.
5. Kutangaza na kuuza bidhaa za kampuni, malengo na maono ya kampuni kitaalam
6. Kuandaa Mkakati bora wa biashara na mipango ya muda mfupi na muda mrefu
7. Kubuni kitaalam namna kuwekeza, kuboresha kampuni ili kuongeza faida kwa kampuni na kujenga imani kwa wadau wa kampuni ya Luhira na wakurugenzi
8. Kuandaa Operational Manuals za kampuni.
9. Kuanda bujeti ya mwaka na taarifa za robo, nusu mwaka na mwaka

Mshahara: Mshahara mzuri utatolewa kwa atakayepata nafasi hii

Cheo: **Afisa Masoko(Marketing Officer) - Nafasi 1**
Mwajiri: Bodi ya Wakurugenzi
Kuwajibika kwa: Afisa Mtendaji wa Kampuni
Kituo cha Kazi: Songea

Kazi na Majukumu ya kazi ya Afisa Masoko.

1. Kutafuta masoko ya kampuni.
2. Kuweka mpango kazi wa muda Mrefu na Mfupi wa kupata, na kutumia masoko ya kampuni.
3. Kutoa report za kila Wiki na Mwezi ama kulingana na maelekezo ya Ofisi, au pale zitakapo hitajika.
4. Kuongeza masoko na namna ya kusimamia masoko yaliyopo ndani ya kampuni.
5. Kazi nyingine kama zitakavyo pangwa ama kuelekezwa na kampuni.

Sifa za Mwombaji

1. Awe na Shahada (Degree) ama Diploma ya masoko kutoka katika chuo kinachotambulika.
2. Awe na uwezo mzuri wa kuongea na kuandika Kiswahili na Kingereza.
3. Awe na uwezo wa kutumia kompyuta vizuri katika program za window.
4. Awe na uzoefu usiopungua angalau miezi sita.

Mshahara : Mshahara mzuri utatolewa kwa atakayepata nafasi hii

Cheo: **Mhasibu wa Kampuni Nafasi - 1**
Mwajiri: Bodi ya Wakurugenzi
Kuwajibika kwa: Afisa Mtendaji wa Kampuni
Kituo cha Kazi: Songea

Kazi na Majukumu ya Mhasibu

1. Kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya Kampuni
2. Kushirikiana na Mhasibu kuandaa taarifa za maduhuli;
3. kufanya usuluhisho wa hesabu za benki na nyingine zinazohusiana na masuala ya fedha
4. Kuandaa taarifa mbalimbali za mishahara;
5. Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi;
6. Kutunza daftari la amana; na
7. kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi

Sifa za Mwombaji

1. Awe na “Intermediate Certificate” (Module D) iliyotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na NBAA;
2. Awe na Shahada ya Biashara/Sanaa aliyejiimarisha kwenye fani ya Uhasibu
3. Awe na Stashahada ya Juu ya Uhasibu kutoka Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali

Mshahara : Mshahara mzuri utatolewa kwa atakayepata nafasi hii

Cheo: **Fundi Mchundo(Useremala- Carpentry) Nafasi - 1**
Mwajiri: Bodi ya Wakurugenzi
Kuwajibika kwa: Afisa Masoko
Kituo cha Kazi: Songea

Kazi na Majukumu ya Fundi seremala

1. Kuchambua na kushauri juu ya matumizi ya aina mbalimbali ya mbao
2. Kutengeneza samani na mazao yatokanayo na mbao
3. Kufanya ukarabati mbalimbali wa samani na kazi zinahusu mbao
4. Kukagua na kutoa taarifa ya maeneo yanayohitaji matengenezo
5. Kushirikiana na wafanyakazi wengine katika kutimiza malengo ya kampuni
6. Awe anajua aina za mbao na vifaa vya fundi seremala
7. Kufanya kazi nyingine kama utakavyolekezwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni

Sifa za Mwombaji

1. Elimu ya kidato cha nne na Cheti cha Ufundi Stadi (Trade Test Grade III/CBET I) yenye mwelekeo wa Useremala –‘Carpentry kutoka VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
2. Mwombaji awe amehitimu kidato cha nne IV katika masomo ya Sayansi na ufuzu mafunzo ya Ufundi katika fani ya Ufundi Seremala katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali
3. Aliyemaliza kidato cha nne wenye Cheti cha majaribio ya Ufundi Seremala Hatua ya pili kutoka Chuo cha Ufundi Seremala kinachotambuliwa na Serikali
4. Awe na uzoefu wa kazi na aeleze sehemu alizowahi kufanya kazi alizofanya

Mshahara : Mshahara mzuri utatolewa kwa atakayepata nafasi hii

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 au zaidi.
2. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na picha (passport size) ya hivi karibuni.
3. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika kama vile:-
4. Mwombaji aambatanishe picha ndogo mbili (passport size) za rangi katika barua yake ya Maombi.
5. Waombaji wawe hawajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai.
6. Maombi yote yaambatanishwe njia za mawasiliano kama vile namba za simu, barua pepe au anwani za makazi.
7. Mwombaji anatakiwa kuambatanisha viambatanisho vyote muhimu.

Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

Mwenyekiti wa Bodi
Ruhira Company Limited
S.L.P.80
Songea- Tanzania
Barua pepe: luhiracl2022@gmail.com

Mwisho wa kupokea Maombi ni tarehe 4/12/2023 saa 09:30 alasiri
